# *Mara Nyingine Tena*

Asante, sana. Na tuombe.

Baba wa Mbinguni, tumekusanyika tena katika Jina la Mtoto Wako mpendwa, Bwana Yesu, kuonyesha upendo wetu katika ibada Kwake tena. Tunaomba ya kwamba Roho Wake atakutana nasi, na kwamba Yeye atatupa kila mmoja sehemu ya huyo Roho ambayo huenda ikatupa neema ya kutuendeleza tuikamilishe safari na kupiga vita vilivyowekwa mbele zetu, vile vita vya Imani. Lijalie, Baba. Na utumegee, alasiri ya leo, Mkate wa Uzima, upate kututia nguvu, kwa kuwa imeandikwa, “Mtu hataishi kwa mkate pekee, bali kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu.” Jalia tusikie hilo, alasiri ya leo, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

2 Ketini. Nikimpongeza Ndugu Carlson, ndio kwanza anikaribishe yapata dakika kumi baada ya wakati. Anafanya vizuri zaidi. Mkutano wa juma lingine, tutaninii tu . . . Huenda nitakuwa hapa kwa wakati ufaao . . . ? . . . Tuna furaha sana kwa ajili ya majaliwa hayo.

3 Sasa usiku wa leo ndio usiku wetu wa kumalizia wa ibada fulani hii, nami ninataka kuwaachilia mtoke kwa wakati mzuri kusudi mweze kula chakula che—chenu cha jioni. Ninajua wengi wenu wanakiita mlo wenu mkuu wa kutwa. Lakini kama nimepata mlo wa kutwa, basi chakula changu cha jioni kitaingilia wapi?

4 Sasa, nilikuwa nikizungumza na jamaa fulani, akasema, “Loo, Ndugu Branham, ni—ni mlo wa kutwa.”

5 “Loo, kweli?” Nikasema, “Ninataka kuthibitisha wewe umekosea.” Nikasema, “Hatuli chakula cha kutwa cha Bwana; tunakula chakula Chake cha jioni.”

6 Kwa hiyo sisi—sisi tunapenda kukiwazia kama Bwana, kama chakula chetu cha jioni, chakula cha Bwana cha jioni usiku ule, si asubuhi wala alasiri. Yeye, Yeye alikikila wakati wa jioni, kilikuwa chakula Chake cha jioni.

7 Sasa, kwa hiyo tunataka kurudi mapema. Na kwa hiyo hatutachelewa usiku wa leo, Ndugu Carlson anaenda kuniingiza tu kwenye wakati ufaao usiku wa leo. “Imani ni bayana ya mambo yatarajiwayo.” Nami sijui, Bwana akipenda, huenda nikajaribu kuzungumza usiku wa leo, kama ninaweza kupata kidogo, muda wa kutosha, juu ya, *Kuhesabu Kinyumenyume*. Ninii, kwa kuwa ni Ujumbe mdogo, wa kisayansi ambao Bwana amenipa kwa ajili ya siku za mwisho. Na labda, Bwana akipenda, huenda nikaweza kuzungumza juu ya hilo usiku wa leo.

8 Sasa, tulikuwa na wakati mzuri sana jana usiku. Nilienda huko, nikasema, “Hatuendi kuwaombea wagonjwa,” na Bwana aliwaponya wagonjwa hata hivyo, mnaona. Amina. Wakati mwingine tunaweza kusema jambo fulani, bali Bwana anaweza tu kuvuruga hilo wakati wowote Yeye anataka kufanya hivyo. Unaona, Yeye—Yeye ni Mungu.

9 Sasa ninataka kusoma upesi kutoka kwenye Maandiko, kwa ajili ya fungu dogo ambalo ni—niliwazia kwamba huenda likawa msaada kwetu alasiri ya leo.

10 Sasa, akiniachilia nianze kwenye wakati ufaao, ninataka kujaribu kuondoka kwenye wakati ufaao, na hiyo itakuwa yapata saa kumi u nusu, ambayo itakuwa yapata dakika hamsini kuanzia sasa.

11 Hebu tugeukie sasa kwenye Kitabu cha Waamuzi, mlango wa 16, na hebu tusome vi—vifungu vya 27 na 28, tunapolitazama Neno.

> *Basi nyumba ile ilikuwa imejaa watu waume kwa wake; na wakuu wote wa Wafilisti walikuwamo humo, na juu ya dari palikuwa na watu elfu tatu waume kwa wake,*. . . tazama *wakati Samsoni alipocheza.*
>
> *Samsoni akamwita* BWANA *akasema, Ee Bwana*. . . *unikumbuke, nakuomba, ukanitie nguvu, nakuomba, mara hii tu, Ee* Bwana, *ili* nipate . . . *kujilipiza kisasi juu ya Wafilisti kwa ajili ya macho yangu mawili.*

12 Na tuombe tena. Bwana Yesu, lichukue fungu hili dogo, na ulimwagie Kanisa maji kwalo, Bwana. Tunaomba na kulikabidhi Kwako, katika Jina la Yesu. Amina.

13 Hapana shaka palikuwa na yapata Wafilisti elfu tatu, wakitazama chini kutoka juu ya orofa ya juu ya uwanja huu mashuhuri, wakati hawa wawili walipoingia uwanjani alasiri hiyo. Hapana shaka ilikuwa siku yenye joto. Siku nzima walikuwa huko nje. Basi katika umati huu mkubwa, juu ya ulingo huu mkubwa ambao ulijengwa kitu katika utaratibu wa uyoga uliowekwa juu-chini; na kizingiti kikuu katikati, kilichoenda kitu kwa namna *hii*, na kushikilia vizingiti viwili vilivyowabeba watazamaji wote kote; majemedari wa vita waliojikwatua na wanawake wao waliopambwa kwelikweli. Wote waliinama mbele kwenye tafrija hii, kwa kuwa walitaka wapate kuona vizuri, kile ambacho kilikuwa kinatendeka.

14 Kulikuwa na vitangulizi, burudani yote. Labda walikuwa na tumbili wadogo ambao—ambao walifanya sarakasi ndogondogo. Pia walikuwa na vitu mbalimbali ambavyo walijiburudisha kwavyo, mapigano, mwereka, na—na—na labda mapigano ya watu wawili kwa upanga hata kufa, na vitu vingine vingi ambavyo—ambavyo walikuwa wamejiburudisha kwavyo siku nzima, kwa kuwa ilikuwa ni siku kuu, lakini sasa tukio lenyewe liliwadia.

15 Mnajua jinsi sisi sote hungojea kwa subira huku vitangulizi vikiendelea. Nao wanangojea tu—tukio lenyewe, na hapo ni wakati kila mtu anapoketi na kutazama. Tunalitazama katika ibada zetu za kidini, wakati tunapokuwa na u—uimbaji wetu, na shuhuda zetu, na mahubiri, na kadhalika; bali tukio lenyewe ni kuona kile Bwana anachoenda kufanya, kuona kile ambacho kimemfanya Yeye kutukusanya pamoja. Sote tuko chini ya matarajio kuona tu kile mwisho unaoenda kuwa, tukio lenyewe. Ni hivyo katika kitu chochote. Daima tunatazamia tukio lenyewe.

16 Ndipo wote wakasimama kutazama mbele, kuona kilichokuwa kinaendelea, kwa sababu tukio lenyewe lilikuwa linaletwa kwao, nao waliona nini ila mtu kipofu akiongozwa na mvulana mdogo.

17 Kumbi zilikuwa na mwangwi alasiri yote, pamoja na shamrashamra za ulevi, jinsi ambavyo walipitisha wiski na vinywaji vyao ghali; na wanawake wao warembo, waliojipaka rangi na kujipamba, na majemedari wa vita mashuhuri wenye vyeo, na wote. Ilikuwa ni sherehe kubwa. Walikuwa wanasherehekea ushindi. Loo, jinsi ninavyochukia kusema hili! Ushindi ambao mungu-samaki Dagoni alikuwa amepata, dhidi ya mtumishi wa Mungu. Inaenda tu moja kwa moja mpaka chini yangu, kunibidi kusema hilo, bali ni kweli. Wakisherehekea kwa njia kama hiyo, ushindi dhidi ya mtumishi wa Yehova. Ni kitu cha aibu jinsi gani! Unywaji pombe, shamrashamra za ulevi, na wanawake waliojipaka rangi, na kujipamba, na watu mashuhuri wenye vyeo, mioto ilikuwa inawaka chini ya mungu-samaki, na ni sherehe ya jinsi gani hapana shaka hiyo ilikuwa.

18 Lakini sehemu ya kuvunja moyo, kama maelfu ya miaka baadaye kwamba inatubidi kuwazia nyuma kuhusu tukio kama hilo, na wakati Mungu mkuu wa Mbinguni, Yule aliyekuwa amekusudia moyoni Mwake kuangamiza taifa hilo kwa sababu walikuwa makafiri, na alikuwa amemtuma mtu kuifanya kazi hiyo, na hapa sanamu ya mungu-samaki ilikuwa inasherehekea ushindi dhidi ya mtumishi wa Yehova. Yehova hakushindwa; mtumishi ambaye Yeye alimtuma kuifanya, alipoteza ushindi.

19 Ni tamasha la jinsi gani, ni jambo la aibu jinsi gani hilo lilikuwa! Mvulana huyo alimwongoza huyo mtu kipofu, anayejikwaa kupita u—ukumbini, hadi kwenye miimo hii mikubwa ya katikati, ambapo uyoga huo mkubwa uliowekwa juu-chini au katika mfano wa mwavuli uliukalia, ambapo watu walitazama chini namna *hii*, kutoka kwenye vitu kama nguzo chomozi zikienda juu na kushikilia kitu hicho pamoja, limejengwa kwa jiwe ambalo haliwezi kutengenezwa tena leo. Hakuna mtu angaliweza kulijenga namna hiyo. Lakini ni kitu kikubwa jinsi gani hicho kilikuwa! Na maelfu ya makasisi wenye sifa ambao walikuwa wametumikia sanamu, huku wametanua vifua vyao nje kabisa, na sherehe zao zote na desturi za ibada juu

ya sanamu yao, kwamba alikuwa amemshinda Yehova. Ni siku kuu jinsi gani hiyo ilikuwa, unywaji, shamrashamra za ulevi, na kufanya yasiyofaa!

20 Basi huyu hapa anakuja mtumishi wa Yehova, kipofu, anajikwaa, akiongozwa na mvulana mdogo, kuja kwenye nguzo hii kuu, kufanya mchezo. Tukio lenyewe la burudani lilikuwa ni kufanya mchezo kutoka kwa kusudi la Yehova lililoagizwa kuangamiza taifa hilo. Na, hata hivyo, taifa hilo limechukua kitu ambacho Mungu alikuwa ameweka ili kuwaangamiza, na sasa walikuwa wamemteka na walikuwa wanafanya mchezo kutoka kwake, tafrija lao kuu katika sherehe yao.

21 Hilo si karibu linakuua tu, kulazimika kutazama hilo? Kuwazia kile kingeweza. . .Hadithi hii kwa kweli haikupaswa kusimuliwa. Lakini labda ilisimuliwa kwa ajili—kwa ajili ya kutufundisha, imeandikwa hivyo. Amedhalilishwa, amevunjika, amesimama sasa akiwa ameshindwa, moja kwa moja kati ya nguzo mbili zilizoshikilia jengo.

22 Ni mfano wa jinsi gani huo ulio wa kanisa leo hii! Ni mfano wa jinsi gani ulio wa jamii ya watu walioanguka, ambao wamejisalimisha kwa ulimwengu na kitu kile kile ambacho tupo hapa ili kushinda. Kanisa ambalo limesalimisha maadili ya—yake, ambalo limesalimisha Biblia, likasalimisha nguvu zake, likasalimisha kabisa upanga wake, na limesimama limedhalilishwa katika saa ambapo ishara zinazokaribia za Kuja kwa Yesu Kristo zimewadia; wakati linapaswa kuwa limeoshwa, bila waa wala kunyanzi, likisimama kumpokea Bwana-arusi wake.

23 Ni picha ya jinsi gani tunayoona hapa, mfano wa utovu wa maadili unaokalia juu ya taifa, taifa hili. Na mimi siendi kujaribu kukaa na Maandiko yangu muda mrefu sana, ili niweze kumaliza haraka. Lakini ningeweza kufananisha hilo na kanisa, na taifa, na siasa, pia na kila kitu ambacho unaweza kuweka mkono wako juu yake leo, kando na Biblia ya Mungu. Imeoza kimaadili, jamii yenyewe ya wanadamu, iko tu katika hali mbaya!

24 Na hapo chini ya makafiri na wasioamini ambao wanaweza kunyosha kidole chao usoni mwa kanisa, ambalo linapaswa kuwa na Ujumbe kwa ajili ya siku hii, na kuwauliza, "Haya yote yanamaanisha nini?" Nao hawana jibu. Hawana jibu. Kwa nini? Walifanya kama Samsoni alivyofanya. Wamesalimu amri.

25 Kwa hiyo hebu mwone amesimama hapo, na sisi tungesema, "Basi huyu ni Samsoni?" Hebu tuone picha yake, huyu shujaa mkuu, mwenye nguvu. Hebu tumwone, alasiri ya leo, kwamba alikuwa na mabega mapana, mwili mkubwa. Na hapa jitu hili kubwa la mtu limesimama hapo, kipofu, amefungwa na kamba ndogondogo, na kuongozwa hadi katikati ya sakafu, amedhalilika, amevunjika, ameshindwa, huku Mungu mkuu

wa Mbinguni akiangalia chini juu ya hali hiyo. Hapa chini, wapinzani wake, askari walevi wakitazama chini.

26 Ningewazia, waliposimama hapo, Wafilisti wengi hata walikuwa wametetemeka katika viatu vyao, kusikia jina lake. Samsoni lilikuwa ni jina lenye nguvu, wakati mmoja; vivyo hivyo na Ukristo, kanisa lilikuwa. Na mimi ninaenda kulifananisha na kanisa, onyesho hili. Jina Samsoni, watu walizimia tu, kwa kuwa alikuwa namna fulani ya mtu ambaye hawakuwa wamemwona mtu kama huyo. Nguvu zake zilizidi chochote ambacho ulimwengu uliwahi kuwa nacho. Hakuna kitu walichokuwa nacho kingelinganishwa nazo. Wengi walimkumbuka walipokuwa wanamtazama amesimama pale katika hali hiyo.

27 Wengi walimtazama kutoka kwenye orofa za juu na kukumbuka kumwona akisimama katika mahali pengine. Siku moja, akiwa amesimama na mfupa wa taya la nyumbu, mkononi mwake, huku Wafilisti elfu moja wamemzunguka, walipokuwa wamekimbilia miamba kwa ajili ya usalama; amesimama, akaashiria kwa vidole vyake, "Njoni, kama mnataka baadhi yake!" Lakini sasa hebu mwangalie.

28 Wengi wa Wafilisti, usiku huo mmoja alishawishiwa kuingia na kahaba na katika m—mji wa Gaza, walichukua malango makubwa mazito ambayo yangekuwa na uzito wa tani nyingi, na kumzingira ndani kwa uzio na kumshika, na kutuma taarifa kwa askari na kusema, "Sasa tumemshika. Tumemfungia ndani." Kama ibilisi daima anavyojaribu kufanya, kukufungia ndani ya kitu fulani.

29 Lakini kumbuka wakati Samsoni alipoamka kesho yake asubuhi, ama usiku huo, hasa, kuona kwamba alikuwa amefungiwa ndani. Angeweza kugusa nyuma upande wa nyuma ya kichwa chake na bado anajua alikuwa ni mwana wa Mungu wa agano, na hakukuwa na chochote kingaliweza kumfungia ndani. Kanisa wakati mmoja lilisimama hivyo, pia. Alifanya nini? Alisimama, akatembea kuteremka mtaani, akayang'oa malango kutoka kwenye mashimo yake, na kuyaweka juu ya mabega yake na kupanda juu ya kilima na kuketi chini.

30 Wengi wakisimama pale alasiri hiyo walikumbuka tukio hilo. Lakini hebu mwangalie sasa, amepofushwa, amedhihakiwa, mwenye kufuata tu amri za tafrija kwa adui. Nguvu zake zote ambazo alikuwa nazo wakati mmoja kwa ajili ya usalama wake, kwa ajili ya mafanikio ya Mungu aliyokuwa amezaliwa ulimwenguni kufanya, zilikuwa zimevuliwa kutoka kwake na mwanamke.

31 Nafikiri jambo lilo hilo lingeweza kutumika leo hii, kwamba mwanamke anayejifanya kuwa Bibi-arusi wa Kristo, na kuwekea msingi mafundisho yake pamoja na "kikombe cha machafu ya machukizo yake, ya uasherati wake." Amepindua

kikombe cha uasherati wake katika vinywa vya kanisa la Mungu ambalo limeinuliwa kuonyesha ishara Zake na maajabu, kama agizo la mwisho la Yesu lilikuwa lifanye, katika Marko 16. Na sasa tunakuta kwamba amechukua kundi dogo, nyenyekevu la Mungu na kuwaundia dhehebu jinsi tu hasa alivyofanya mwenyewe, na amewafanya kusimama wamevuliwa nguo, wakikana Nguvu zake, wakimkana Roho Mtakatifu, wakikana nguvu za kunena kwa lugha, wakikana Nguvu za—za Roho Mtakatifu kuwafufua wafu, na kuwaponya wagonjwa na kutoa pepo. Na sasa Wafilisti wanakujia wewe, na wewe unaenda kufanya nini sasa, umevuliwa?

Loo, kitu kile ambacho hapana shaka kilipitia niani mwa mtu huyo!

32 Tumeona kile ambacho hapana shaka kilipitia niani mwa Wafilisti. Walikuwa wamemjua. Wakati, nimemsikia mmoja akimkaribia mwingine, labda, na kusema, "Ninakumbuka wakati ambapo ungesema 'Samsoni,' kila Mfilisti angekimbia kama panya kuingia shimoni. Nimesikia wakati, ungesema, watu elfu moja wangekuwa wanatembea taratibu kuvuka jangwa, wanasema, 'Samsoni anakuja,' wangeangusha silaha zao na kukimbilia usalama kwa nguvu walivyoweza."

33 Lakini sasa mwangalie. Yuko katika hali ya kutisha, amefungwa, yote kwa sababu alipatana na mwanamke. Hilo ndilo lililoleta hayo. Huyo mwanamke alimvua nguvu zake. Alishikilia kujaribu kutafuta mahali nguvu zake zilipokuwa. Alijua yeye alikuwa ni mtu mkubwa, lakini walikuwa na watu wakubwa, pia. Lakini huyu Delila, alikuwa ni Yezebeli kweli—kwelikweli. Alijua jinsi ya kumshughulikia, ili kumvuta kwake na kusema kwamba (yeye) alimpenda. Bali, wakati wote, alikuwa akijaribu kutafuta kote, ambapo nguvu zake zilikuwa.

34 Na hilo ndilo jambo lile lile ambalo Yezebeli amelifanyia kanisa, limetafuta kote mpaka limegundua mahali nguvu zake zilipo. Na nguvu ziko katika Neno. "Neno ni Mungu." Basi hatimaye aligundua mahali nguvu hizo zilipokuwa, ndipo akampeleka huko chini Nikea, Rumi, na kunyoa vishungi vyake. Na sasa wamechukua kilichosalia kutokana na hilo, na kuwarudisha katika Baraza la Makanisa Ulimwenguni, na kunyoa vishungi vyao tena. Ni kunyoa kila mara, kuondoa *Hili*, na, "*Hili* halimaanishi *lile*. Siku za miujiza zimepita. Hakuna kitu kama *hiki, kile, kinginecho*." Wao, waligundua mahali nguvu zilipokuwa, wakiweka mabatizo na kupeana mikono na mambo haya yote mengine, badala ya Neno la Mungu la kweli lisilogoshiwa.

35 Neno hili ni Mungu, ambalo lilipewa Kanisa Lake kuushinda ulimwengu na pepo, na ugonjwa, na kutorosha pepo, na hakuna dhehebu lililopewa Kanisa. Kanisa lilipewa Neno; Hilo ndilo nguvu zake. Lakini wamekata *Hili* na kuondoa, wamekata *Lile*

na kuondoa, na wamenyoa na kutoa kishungi *Hiki*, na kunyoa na kuondoa kishungi *Kile*, mpaka amesimama amenyolewa leo hii, kama sista wa Katoliki, amenyolewa, mpaka amekubali lundo la kanuni za imani zilizobuniwa na mwanadamu kwa ajili ya fundisho lake, hasa tu kile nabii alisema angefanya. Naye huyu hapa amesimama leo hii, amedhalilika. Wakati Mungu wa Mbinguni amewachagua wavua samaki wasio na elimu, na kadhalika, na ameshuka ndani ya hao na kuthibitisha Hilo, kwamba Yeye angali anabaki Mungu, nao hawawezi kutoa jibu kwa kusanyiko lao kwa Hilo kwa sababu halijaunganishwa na dhehebu lolote. Basi amesimama amedhalilika, ambapo anapaswa kuwa amesimama katika nguvu zake.

36 Laiti kanisa leo hii lingesimama kama lilivyosimama kwenye Siku ya Pentekoste, laiti kanisa leo hii lingesimama kama lilivyosimama katika siku za Ireneo, na katika siku za Mtakatifu Martin, ama katika siku za Polycarp, ambapo Kanisa lingetembea taratibu moja kwa moja kuingia mautini kabla ya kuweza kuliasi Neno lolote la Mungu! Ireneo, Martin, watu hao wote, walishikilia imara kwenye huo ubatizo wa maji katika Jina la Yesu Kristo. Kila mmoja wao alishikilia imara kwenye huo ubatizo wa Roho Mtakatifu, manabii, ishara na maajabu.

37 Nao wameliondokea leo hii. Ni nini kilichofanyika? Delila alijua mahali nguvu zilikuwa. Na kama angeweza kuondoa seminari hizo kwenye hilo Neno, kuenda kwenye theolojia fulani ya kubuniwa na wanadamu, alikuwa nayo, basi ilikuwa rahisi kuwafunga na kuwaelekeza katika Baraza la Makanisa Ulimwenguni, baraza hili la ekumeni.

Unasema, “Huna haki yoyote.”

38 Ningali mwananchi wa Marekani. Nina haki ya uhuru wa kunena. Hiyo ni kweli. Hakika niko hivyo. Tazama, hiyo ni Kweli kabisa.

39 Loo, jinsi hapana shaka alivyojihisi, kile kilichopitia niani mwa mtu huyo, wakati aliposimama pale, kipofu!

40 Sasa, Yezebeli alijua, ama si Yezebeli, bali Delila alijua, kama angeweza kuyang’oa macho yake, hilo lilitosha.

41 Na hilo hasa ndilo Delila wa siku hii ya mwisho amefanya kwa kanisa, kuyang’oa macho yake, kwa ahadi ya Mungu, na kuwauzieni dhehebu fulani kubwa la kiakili. Kila mtu anapenda kununua, . . . sema, “Mimi ni mfuasi wa kanisa la Kwanza. Mimi ni mshiriki wa *hapa* chini. Mimi . . .” Unaona, mradi tu ibilisi anaweza kuyang’oa macho yako, kwa Neno la Mungu na ahadi ya Mungu! Haijalishi jinsi inavyosikika ya kipumbavu, ni ahadi ya Mungu.

42 Sasa, siungu mkono dini potovu, si hata kidogo, lakini hizo dini potovu zinajulikana kwa kazi zake. Vivyo hivyo na Kanisa la Mungu linajulikana kwa kazi Zake. Bali ninajaribu kusema kile ambacho Delila amemtendea Samsoni.

43 Sasa hebu tuchukue upande wa Samsoni, kile ambacho hapana shaka kilipitia niani mwa mtu huyo wakati akisimama hapo. Ushindi wote mkuu ambao alikuwa nao wakati mmoja, hapana shaka ulipitia niani mwake. Tukio linaendelea sasa, burudani ya alasiri inakaribia kuanza. Wale wanaopaswa kuburudishwa wanawaza kuhusu kile alichokuwa, naye huyu hapa amesimama akiwazia kile alichokuwa. Lakini kwa sababu mwanamke fulani alimshawishi, picha imebadilika, kwa kile ilichopaswa kuwa. Mungu alimwinua Samsoni kuangamiza taifa hilo, hilo lilikuwa ndilo kusudi hasa la kumleta.

44 Ikiwa Mungu anaweza tu kumpata mtu mmoja, hayo ndiyo yote anayohitaji Yeye, mtu mmoja ambaye anaweza kujisalimisha kikamilifu Kwake. Yeye hachukui jeshi; Yeye kamwe hakuwahi kutumia hilo. Yeye humtumia tu mtu.

45 Sasa, Samsoni alimpa Mungu nguvu zake kutumia, bali hakumpa Mungu moyo wake. Alimpa moyo wake Delila, na kumpa Mungu nguvu zake.

46 Lakini inakubidi kusalimisha nafsi, mwili, roho, nguvu, kila kitu ulicho, kwa mapenzi ya Mungu, uwe mfungwa Kwake. Utakuwa mfungwa wa mtu fulani. Wewe si mali yako mwenyewe. Wewe ni mfungwa wa mtu fulani. Ama wewe ni mfungwa wa ibilisi, ukijua Kweli hii na usijisalimishe Kwake, au mfungwa kwa—kwa ulimwengu, na kujisalimisha kwa Mungu, mmoja au mwingine. Ama wewe ni mfungwa wa ibilisi, kwa dhambi, au wewe ni mfungwa wa Mungu, kwa haki. Wewe ni mmoja au huyo mwingine.

47 Basi sasa Samsoni anawaza kuhusu ushindi mkuu ambao alikuwa amepata. Hapana shaka ilimjia niani kuhusu jinsi, kwamba wakati alipokuwa mvulana mdogo, kwamba Mungu alikuwa amemthibitisha, akamwambia mama yake jinsi ambavyo kwamba inampasa kufanya; asinywe vileo, ama—ama achunge chakula chake, kwamba alikuwa anamkuza Mnadhiri. Jinsi alivyochana nywele zake, na kumwambia, "Mwanangu, kupitia vishungi hivi, ni agano na Mungu, kwamba nguvu zako zitakaa humo. Usije, kamwe ukaitoa. Usije, kamwe ukaitoa siri yako. Kamwe, usiisalimishe. Chochote ufanyacho, kaa nayo."

48 Yesu Kristo aliliambia kanisa, kwamba, "Mbingu na nchi zitapita, bali Neno Langu halitapita kamwe. Na yeyote atakayeondoa Neno moja kutoka kwa Hilo, au kuongeza neno moja kwenye Hilo, sehemu yake itaondolewa kutoka kwenye Kitabu cha Uzima." Kanisa linapaswa kuwazia hilo sasa wakati tunaposimama katika machafuko haya, katika saa hii maombi tu . . . kabla ya Kuja kwa Bwana Yesu, dakika yoyote, kwa ajili ya Unyakuo.

49 Ushindi mkuu ambao tunaweza kurejea nyuma, katika siku zilizopita, katika marekebisho, nyuma katika siku za Ireneo na Mtakatifu Martin, Patrick, na wale waliopinga madhehebu hayo.

50 Basi wakati Luther alipojitokeza na kupinga lile dhehebu la kwanza, kanisa Katoliki, na kundi ambalo lilimfuata lilirudi nyuma moja kwa moja na kuunda dhehebu nyuma yake.

51 Wakati John Wesley alipotoka katika Uanglikana, na, punde tu Wesley alipoondoka, waliunda dhehebu moja kwa moja nyuma yake.

52 Na Pentekoste ya mwanzoni ilitoka katika madhehebu. Hilo lilikuwa ni neno lililolaaniwa kwako. Lakini, "Kama mbwa anavyoenda kwenye matapiko yake, na nguruwe kwenye kugaagaa kwao," mmerudi moja kwa moja katika kitu kile mlichozaliwa kukishinda. Haleluya! Hilo huumiza moyo wangu, pia, hata zaidi ya kuwaza kuhusu ushindi kule ambako Dagoni alikuwa nao dhidi ya Samsoni. Ninaona kile Yezebeli alicho nacho juu ya kanisa. Na hiyo ndiyo sababu kwamba kila nguvu na kila mshipa katika mwili wangu, ninajaribu kukipinga kitu hicho, na kuita hilo kanisa lirudi mahali pake pa toba. Mama zenu, baba zenu, walifukuzwa kutoka kwenye hayo madhehebu. Walitoka ndani yake na kulipinga, na hapa watoto wao wamerudi moja kwa moja kuzunguka na wamerudi moja kwa moja ndani ya kitu kile hasa walichotoka ndani yake. Kama hiyo si picha ya Samsoni, kile Delila alichofanya!

53 Jinsi tunavyopaswa kuachilia mawazo hayo yapitie niani mwetu, ya ushindi mkuu. Sina muda wa kuufikia, na kutimiza neno langu kwenu.

54 Na la Mungu, alikuwa amemwinua kwa kusudi hili, naye hapo amesimama kati ya miimo hiyo miwili, kipofu, ameshindwa, na kudhalilika. Alikuwa angali mwili ule ule mkubwa aliowahi kuwa, ila nguvu zake zilitoweka.

55 Kanisa ni kitu chochote, lina nguvu zaidi katika washiriki kuliko lilivyowahi kuwa. Lakini liko wapi Neno, nguvu, zikidhihirishwa? Zimekatiliwa mbali kutoka kwenu, na madhehebu yenu yanyoayo nguvu.

56 Alikuwa amemuaibisha Mungu. Si tu kwamba alikuwa amempungukia Mungu, bali aliwaaibisha watu wake mwenyewe. Alikuwa ameshindwa kabisa. Sasa alikuwa ni mfungwa wa taifa lile lile ambalo Mungu alimwinua kuangamiza.

57 Na hapa linasimama dhehebu la mwisho la kanisa, Pentekoste, alasiri ya leo, limeshindwa tu kama Samsoni alivyokuwa. Huenda usiamini hilo. Lakini ikiwa utafungua tu nia yako kwenye Neno, utaona kwamba ni Kweli.

Walimfanya kufanya vitimbi, kwa ajili ya burudani.

58 Jinsi wakati mwingine nilisema, si muda mrefu uliopita. Hawa Wafanyabiashara wa Full Gospel, kadiri ninavyowapenda, na katika jarida lao, wakiandika, "Mtakatifu Kasisi Baba *Fulani-wa—fulani*." Enyi maskini Wapentekoste,

vipofu, waliodanganywa! Mna shida gani? Hivi hamjui Mwokozi wetu alisema, "Msimwite mtu yeyote hapa duniani, 'Baba'?" Hivi hamtambui ibilisi anamchukua tu mtu fulani ambaye amefukuzwa kutoka katika moja la hayo huko, hapa nje, na kuwafanya tu kitu cha kuchekwa? Hawaingii ndani. Msiache mtu yeyote awaambie kuwa wanaingia ndani.

59 Kuna shida gani na kanisa hili lililodanganywa? Ulimwengu umetoboa macho yake. Hivi hamjui Yesu alisema hilo lingefanyika? Na wakati bikira aliyelala alipokuja kununua mafuta, kamwe hakuyapata. Huyo hapo bikira aliyelala, Lutheri, Methodisti, Presbiteri. Hawayapati. Huenda wakanena kwa lugha na kuruka, lakini hilo halimaanishi chochote. Nimeona makafiri wakifanya jambo lilo hilo, na waabudu shetani, wakinena katika lugha na kuruka, na kuimba na kupaza sauti; kunywa damu kutoka kwenye fuvu la kichwa cha binadamu, na kumwita ibilisi na kunena katika lugha. Kamwe usiegemee mhemuko. Ni Neno la Mungu ndilo halipiti.

60 Huyo hapo, ameshindwa, kama tu na Samsoni alivyoshindwa, akifanya vitimbi sasa. Jinsi Shetani anavyosimama na kuwacheka, kasema, "Angalia, wanadai wanaamini Biblia. Angalia!" Akiwaambia Malaika wote wa Mbinguni, "Angalia, angalia, wao—wao—wao—wao, naam, hao ni waaminio wa Biblia, kila mmoja wao, waangalie wote wakija pamoja. Ninaenda kuwatupa, kila mmoja, huko, kwa hakika kabisa." Anaenda kuwaelekeza moja kwa moja ndani, hasa kabisa kile Maandiko yaliyosema. Inawabidi kufanya hivyo. Hao hapo, wameshindwa. Delila; macho yametobolewa kwa hiyo hawawezi kuiona Kweli.

61 Yesu aliwaambia Mafarisayo, "Mnayo macho, na hamwezi kuona. Mnayo masikio, na hamwezi kusikia." Kwa nini? Kasema, "Maana Isaya alisema hivyo." Alirejea nyuma kwenye Neno, nabii. Mungu Mwenyewe, Yesu Kristo, alirejea nyuma kwenye Neno la nabii Wake.

62 Pia, leo hii, Roho Mtakatifu anarejesha nyuma kumbukumbu yenu. "Wakaidi, wenye kiburi, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu," wanawake, waliojipaka rangi nyusoni, wanavaa kaptura, wanatenda kama ulimwengu, wakikata nywele zao, na kufanya kadhalika, "wenye mfano wa utauwa, bali wakikana Nguvu zake." Vema, kazi zenu wenyewe zinathibitisha kwamba hamwamini. Roho Mtakatifu, katika Neno, akielekeza moja kwa moja kurudi kwenye Neno tena.

63 "Loo," unasema, "Ninaye Huyo." Ukimeza dawa kwa ajili ya ugonjwa fulani, kama haionyeshi, afadhali ubadilishe dawa yako, utakufa katika dhambi zako.

64 Taifa, kusudi hasa, kitu hasa ambacho waliinuliwa kuangamiza, Samsoni, sasa ni mhanga.

65 Vivyo hivyo na kanisa! Liliinuliwa kutia katika aibu, umadhehebu na ulimwengu katika madhehebu, nanyi mmeingia moja kwa moja ndani ya dhehebu. Na kwa kufanya hivyo, hamwezi kufuata Maandiko, kila moja lao lina wazo tofauti, kwa hiyo mlipoteza nguvu zenu. Huyo ibilisi apofushaye!

66 Kuuachia ushawishi wa mwanamke kumwondoa kwenye—kwenye Neno la Mungu. Sasa unasema, “Ndugu Branham, haikuwa hivyo.” Lilikuwa ni Neno la Mungu. Delila alimwondoa Samsoni kwenye Neno la ahadi.

67 Vivyo hivyo na Yezebeli wa siku hii ameliondoa kanisa, akalishawishi kutoka kwenye Neno la ahadi, Biblia Takatifu ya Mungu. Loo, jambo lile lile, jambo lile lile hasa! Walifanya nini? Kumwacha Yezebeli, aliyezungumziwa katika Ufunuo 17, Ufunuo, mlango wa 17, kanisa Katoliki limewakilishwa hapo. Nao wanakuambia kuwa ni wao, pia. Hawaninii. . .Kitabu chao wenyewe kinasema hivyo. Hawaogopi hilo. Ni wangapi wamewahi kusoma maandishi yao wenyewe? Mnajua kwamba hilo ni kweli. Wanasema kanisa Katoliki limewakilishwa. Hiyo ni kweli. Pia kumbukeni, “Yeye alikuwa ni mama wa makahaba. Alikuwa ni kahaba, na mama wa makahaba.” Unaona, ilibidi iwe ni makanisa; si wavulana, ilikuwa ni wasichana, makanisa ya Kiprotestanti, “mama wa makahaba.” Punde tu walipojiundia dhehebu, walifanya jambo lile lile walilofanya kule, walijivua wenyewe kutoka kwenye Neno, na inawabidi kufuata amri za dhehebu fulani.

68 Ninajua hili halipendwi na wengi, bali ni Kweli. Sina vipindi vikubwa vya redio na vipindi vya televisheni, kuungwa mkono. Mungu anisaidie kamwe nisiwe navyo. Ninataka tu kitu kimoja, na hicho ni kuungwa mkono na Yesu Kristo, kwa Neno Lake. Hebu Yeye athibitishe kwamba ninasema Kweli, kwa Neno Lake; si kitu fulani kipotofu, bandia, cha kutokuamini; bali Roho Mtakatifu halisi Mwenyewe, Yule achukuaye ahadi ya siku hii na kuonyesha kwamba ni Kweli. Hayo ndiyo yote ninayotamani kuona. Kama Yesu alivyosema, “Kama sizifanyi kazi za Baba Yangu, basi msiniamini Mimi.”

69 Sasa vipofu! Loo, mnasema, “Sisi si vipofu.” Nyinyi ni vipofu! Biblia ilisema mlikuwa hivyo. Kila msomaji wa Maandiko anajua kwamba huu ni Wakati wa Kanisa la Laodikia. Ni wangapi wanaamini hilo? Halafu, Biblia ilisema kwamba, “Kanisa la Laodikia lilikuwa kipofu, uchi, wala hawakujua.” Hiyo hapo sehemu iliyo mbaya, hata hajui. Yeye ni mbaya kuliko nyakati zingine zote za kanisa zikiwekwa pamoja.

70 “Fahali anajua hori ya bwana wake, au zizi, naye nyumbu anajua zizi lake, na,” Yeye alisema, “Watu Wangu hawajui.”

71 Vipofu, vipofu kiroho! Vipofu kwa kitu gani? Neno la Mungu. Vipofu tu kama wawezavyo kuwa, nao hawataki kuona Hilo. Basi ukiwaambia; watasema, “Loo, naam, ni—ninakusudia

kufanya hilo," lakini hakuna mmoja wao anayefanya hilo. Hawawezi kulifanya na kudumisha ushirika wao katika dhehebu; watawafukuza moja kwa moja kutoka kwake.

72 Huyo hapo amesimama, Delila amenyoa vishungi vyake. Sasa yeye ni—yeye amekatwa nywele; kama wanawake ndani yake, kitu kile kile. Sasa waangalie, wameshindwa, kama tu walivyokuwa.

73 Wahudumu, wajumbe wa kipentekoste wa siku za mwanzoni, usingeweza kuwafanya wanaume hao kuamini kwamba watoto wao wenyewe wangeunda seminari, ambazo walizikosoa, kwa Neno la Mungu, na kutoka ndani yake. Hiyo ni kweli. Ni kitu gani, ambacho tumepata, kupitia seminari hizi? Wameingiza ulimwengu kanisani. Maskini mhudumu mmoja alizoea kuimba:

> Tulilegeza mambo,
> Tukapatana na dhambi.
> Tulilegeza mambo, kondoo wakatoka,
> Lakini mbuzi waliingiaje ndani?

74 Mlilegeza mambo, mkaondoka kwenye Neno. Wakati Hawa alipolegeza kamba, kwa hoja za kiakili za Shetani, kifo kiliingia; na fito ambazo Mungu alikuwa amemzuilia nazo, zilikuwa ni Neno Lake la ahadi. Na sisi tumebadilisha kitu kingine, kanuni ya imani, badala ya Neno. Amina. Mnajua hilo ni Kweli.

75 Tumepata nini, watu wa Kipentekoste leo hii? Kina Riki wengi kupita kiasi. Neno hilo, Elvis na Ricky, kamwe hukusikia kuhusu hilo katika siku zingine. Ni neno, ndilo jina kwa ajili ya siku hii. Huambatana na hili. Linamaanisha jambo fulani.

76 Unasema, "Jina halimaanishi chochote." Basi ni kwa nini Yeye alibadilisha jina la Abramu, kuwa Ibrahimu? Ni kwa nini Yeye alibadilisha jina la Sauli kuwa Paulo? Jina la Simoni kuwa Petro? Ni kwa nini Yeye alibadilisha Jina Lake Mwenyewe?

77 Ni kwa nini Yeye alibadilisha Yakobo kuwa Israeli? Si mpaka alipopigana mwereka na Bwana, si mpaka aliposhinda. Basi wakati Yesu aliposhinda kifo, kuzimu na kaburi, Biblia ilisema, "Alikuwa na Jina jipya." Pia wakati Yakobo aliposhinda.

78 Na iwapo Kanisa linaweza kushinda, ataacha kusema, "Mimi ni Mmethodisti, Mbaptisti, na Mpresbiteri." Wakati anapoweza kushinda kanuni zake za imani na ulimwengu ambao umemvuta humo ndani, atarudi kuwa Bibi-arusi wa Yesu Kristo, Bibi Yesu Kristo. Amina.

Ni tamasha la huzuni jinsi gani, tunapomwona Samsoni amesimama hapo!

79 Wanawake wenye nywele fupi, wakivaa kaptura, nyuso zilizopakwa rangi; na Wapentekoste, wakijiita wenyewe Wakristo, wakiimba katika kwaya.

80 Nilikuwa katika Pentecostal Assembly si muda mrefu uliopita, katika mji mkuu ambapo mtu maarufu, mashuhuri

anakoishi. Na mikutano ikawa mikubwa sana, ilinibidi kuipeleka mahali pakubwa, nao walikuwa na kwaya ya Kipentekoste iliyochaguliwa. Nao hawakujua nilikuwa nimeketi chini moja kwa moja nyuma ya pazia, nikiomba. Na hapo kila msichana katika safu hiyo ya yapata wasichana thelathini na watano, na wavulana thelathini na watano, kuimba *Yule Masihi,* walikuwa wamejipodoa na kukata nywele zao. Ndipo wakati David duPlessis alipokuwa akichukua matoleo ya umishenari, walikuwa wanatenda kana kwamba walikuwa ni Bartimayo kipofu, wakikimbia huku wakipitisha kikombe. Hao ni wajukuu wa Kipentekoste. Huyo si mtumishi wa Kipentekoste wa Mungu aliye na ubatizo wa Roho Mtakatifu. Roho Mtakatifu hatadhihaki Neno Lake Mwenyewe. Hawezi, na abaki kuwa Roho Mtakatifu. Lakini hapo ndipo mmefikia. Loo, Samsoni, anza kuwaza kidogo!

81 Kumbukeni, kanda hizi zinarekodiwa na kutumwa kote ulimwenguni. Sizungumzi tu kwa kundi hili hapa.

82 Samsoni alianza kuwaza kuhusu makosa yake. Loo! Ndipo akaanza kuwaza juu ya kile alichokuwa wakati mmoja.

83 Pentekoste, wazieni kile mlichokuwa miaka elfu moja mia tisa iliyopita. Kanisa, Katoliki, Protestanti, wazieni kile mlichokuwa miaka elfu moja mia tisa iliyopita, na mwangalie kile mlicho leo hii. Chunguzeni kidogo.

Nina yapata dakika nane tu zaidi, ili kutimiza neno langu.

84 Tazameni, lakini wakati alipokuwa amesimama pale, alilia, alianza kuwaza kuhusu makosa yake. Ndipo wakati alipoanza kuwazia kile yeye . . . kilichomtokea . . . Alikuwa kipofu, hivyo basi asingeweza kuona tena, a—amekubali kitu kingine, kwa sababu ya upendo wa mwanamke huyu, huo ndio uliomshika, na ndipo mwanamke huyo akamwangusha.

85 Loo, ni mtego wa jinsi gani ningeweza kuzungumzia hapa, ambao Shetani ameliwekea kanisa. Acha tu macho yako yapofushwe kutoka kwenye Kweli, na, hilo ndilo, wamekupata basi. Na laiti ungalijua tu hilo! Mojawapo ya siku hizi Mungu anaenda kukuthibitishia, kile kilicho alama ya mnyama. A-ha. Tazama, bali mara akipofuka, huyo hapo amesimama.

86 Na hapo alisimama. Ndipo akaanza kukumbuka mambo ya makosa yake, ambapo alikuwa ameiacha njia nyembamba, iliyonyoka, ambapo alikuwa ameondokea ahadi ya Mungu. Ndipo akalia, "Bwana, lipiza kisasi macho yangu!" Ni kwa nini alifanya hivi? Alijua kulikuwa na uwezekano.

Sasa ndipo mahali ninawatakeni msikilize.

87 Samsoni hapana shaka aliwaza kuhusu yote mahali alipokuwa ameiacha njia. Alipaona wakati huo, kumechelewa kupita kiasi sasa. Alipaona, ambapo alikuwa ameiacha njia, ndipo akawaza, "Lazima kuna uwezekano kwamba Mungu

angeweza kujibu." Alijua kama angeweza kutubu na kumfanya Mungu aone kwamba alijutia makosa yake, kulikuwa na uwezekano kwamba Mungu angali angetimiza ahadi Yake.

88 Mungu atafanya hivyo. Anaenda kulifanya. Vile vile sasa, Mungu anaenda kuwa na hilo Kanisa! Usiwe na wasiwasi, Huyo anaenda kuwepo. Roho Mtakatifu atakuwa anatembea hivyo Kanisani mpaka Kanisa na Kristo watakuwa Roho yule yule. Luther alisimama wakati huo kwenye miguu, katika kuhesabia haki; Wesley alisimama katika mdundo wa moyo wa upendo, wa utakaso; bali huu umeinuliwa kufikia kichwani sasa; unaona, zaidi ya hapo. Yeye aliunda dhehebu, ndipo mkulima akaja na kupogoa mzabibu; wakafa, kamwe hawakurudi tena. Kamwe hawatarudi tena. Lakini bado kuna mbegu ya Uzima hapo inayokuja.

89 Bali, tazama, Samsoni aliwazia lazima kuna u—uwezekano. Alilipata hilo wazo.

90 Lakini sehemu ya kuhuzunisha ni kwamba, leo hii, kanisa halishiki hilo. Hawatambui kwamba kuna uwezekano wa uamsho. Hawatambui uwezekano. Hawajalipata ono bado. Wamekaa tu.

91 "Loo," wanasema, "sasa, Ndugu Branham, unafanya nini?"

92 Loo, ninajua mnapiga makofi yenu na kuwa na mikutano mikubwa, na kumetameta na mapambo ya ulimwengu. Inawabidi kwenda kwenye sehemu mashuhuri zaidi. Inawabidi kuwa na burudisho bora, kuliko yote. Inawabidi kufanya *hili, lile,* au *linginelo*. Mchungaji wenu hana budi kuwa na elimu ya seminari pamoja na shahada ya udaktari. Ama, huwezi kuwaambia majirani zenu kule chini kwamba mchungaji wenu ni maskini jamaa fulani kutoka kwenye shamba la mahindi huko nje, aliyepata kuokoka. Yeye ni, "Mchungaji wetu ni Daktari LL.D. *Fulani-wa—fulani*." Kwangu mimi, hilo linamaanisha yeye yuko mbali tu hivyo na Mungu. Hivyo tu, mbali tu namna hiyo, kwa kuwa elimu daima humpeleka mbali. Loo, mnang'ara na elimu.

93 Tena jambo jingine, kuhusu wingi wa huu uinjilisti mamboleo leo hii, kote kuanzia Pentekoste kotekote kurudi nyuma, ni lundo la maonyesho ya Hollywood. Naam, hakika mnametameta na hayo, kama mapambo katika ukumbi wa mungu-samaki Dagoni. Bali hayo mapambo na elimu, na maonyesho ya kiakili pamoja na mng'ao mkubwa, kufanya yeyote wa umati huo asione ushindi wowote na kadhalika, upuuzi huo wote namna hiyo, dhana za kiakili za Injili, na kadhalika, ambazo hazileti Nguvu za Mungu kuwafanya wanawake waache kukata nywele zao, na wanaume kufanya kama iwapasavyo, kuchukua mahali pao katika nyumba na kuwalea watoto wao jinsi inavyowapasa. Haileti Roho wa Mungu.

Samsoni alisimama hapo, mwili mkubwa tu kama alivyowahi kuwa.

94 Nalo kanisa linasimama likiwa na nguvu zaidi katika washiriki kuliko lilivyokuwa miaka arobaini iliyopita, lakini yu wapi Roho wa Mungu? Loo, jamani! Yu wapi Roho wa Mungu ndani yake? Ninaona roho ya Hollywood. Ninaona roho ya ulimwengu. Ninaona roho ya mapambo. Penya moja kwa moja, nimekuwa nikihubiri dhidi yake kwa miaka kumi na mitano, na inazidi tu kuwa mbaya wakati wote. Ninaweza kuiona, na ninaweza kuona roho pale. Lakini yu wapi Roho wa Mungu awezaye kumwelewa Mungu, anayeweza kulitambua Neno Lenyewe wakati Hilo limedhihirishwa, anayeweza kuitambua Kweli? Ni Roho wa Mungu pekee anayeweza kufanya hilo. Hiyo ni kweli. Unaweza kuchukua mapambo, mng'aro, maonyesho.

95 Samsoni alikuwa tu na mwili mkubwa kama alivyowahi kuwa nao, ila nguvu zake zilikuwa zimeondolewa kwake.

96 Kanisa, Pentekoste leo hii, linasimama. Ninaamini, miaka mitatu iliyopita, *Mgeni wa Jumapili* la kanisa Katoliki, lilisema kwamba walikuwa na "wongofu milioni moja kwa Ukatoliki katika mwaka mmoja, lakini kanisa la Pentekoste lilikuwa na milioni moja na laki tano, zaidi ya hapo." Vema, una kitu gani wakati umelipata? Afadhali ningekuwa na watano ambao wangeweza kusalimisha maisha yao kwa Kristo. Yeye anaweza kufanya mengi zaidi na watu watano, au mtu mmoja, aliyejisalimisha, kuliko Yeye angeweza kufanya na milioni arobaini huko nje. Wafuasi wanamaanisha nini? Inamaanisha tu kitu kingine, kwamba mmepofushwa, na kuongeza nguvu zaidi kwa kahaba. Kweli.

Tazama, kanisa leo hii haliko tayari kulipa gharama.

97 Samsoni aliomba aina sahihi ya maombi, "Bwana, jalia nife na adui huyu." Loo, jamani!

98 Haya basi. Hutaki kukifia kiburi chako. Hutaki kuvifia vitu vya ulimwengu.

99 Sasa, kumbukeni, ninazungumza hasa na maelfu kote ulimwenguni, ninaposema hili. Mnaona? Sizungumzi tu hapa Chicago. Ninazungumzia ulimwengu.

100 Hutaki kufa, bali njia pekee ambapo pana uwezekano wa uamsho. Ewe Samsoni uliyepofushwa, hivi huwezi kuona kwamba Delila ameyapofusha macho yako? Na njia pekee utakayoweza kurudisha nguvu kwa kanisa, ni kufa kwa adui ambaye amekuingiza katika hali hii ya kilimwengu.

Samsoni alisema, "Jalia nife pamoja na adui."

101 Ipo gharama kubwa ya kulipa. Lazima ufe kwa kitu hicho kilichokuleta wewe katika kitu hiki. Lazima ufe kwa kitu hicho ambacho kimekufikisha, nyinyi watu wa Kipentekoste, mahali mlipo alasiri hii. Inawabidi kukifia.

102 Samsoni alikuwa radhi kulipa gharama kupata nguvu za Mungu kurudi katika maisha yake tena.

103 Nashangaa kama kanisa, alasiri hii, liko radhi kulipa gharama na kufa pamoja na adui, kitu hicho, umaarufu wako wote, na *haya* yote yako, *yale*, au *mengineyo*, ili tu kuona nguvu za Mungu zikirudi juu yako tena, na kufanyika mfungwa wa Yesu Kristo?

104 Loo, ninasikia baadhi yenu mkisema, "Loo, naam, sisi, tuna miamsho." Bali ni miamsho ya kimadhehebu. Wa Umoja wanataka kuchukua wa Utatu wote na kuwafanya wote wa Umoja. Wa Utatu wanataka kuchukua wa Umoja wote na—na kuwafanya wa Utatu. Church of God wanataka kuchukua kanisa la Mungu la Unabii. Mmoja anataka kuchukua mwingine, kuifanya kubwa dhehe-. . .Hivi hamtambui mnashughulikia tu wanadamu?

105 Sisi ni ndugu. Hakuna dhehebu liwezalo kuutenganisha upendo wa Mungu. Sisi ni ndugu. "Hii watu wote watajua ninyi ni wanafunzi Wangu, wakati mkiwa na upendo mmoja kwa mwenzake."

Unasema, "Ni kwa nini unapiga makelele kuwahusu basi?"

106 Upendo husahihisha. Upendo usiposahihisha, basi si upendo. Ukiona mtoto wako chini barabarani, na usimpe kichemsha tako kidogo, wewe—wewe si baba mzuri. Lakini mama halisi au baba atampindua na kumpiga, amwache ajue inambidi kuondoka barabarani, au aangamie. Huo ni upendo halisi. Bali kusema, "Kadogoo, mpendwa, sijui. Wewe, labda hupaswi kuwa huko nje kwenye wakati huu wa mchana, wakati wa mwisho, ambapo motokaa zinaenda kasi sana." Loo, upuuzi, ewe mhubiri dondoadume, bila ujasiri kuchukua Neno la Mungu na kuita nyeupe nyeupe na nyeusi nyeusi, sahihi sahihi na kosa kosa. Lakini wanafanya hivyo.

107 Naam, tunayo miamsho sawa, lakini hebu angalia maadili yako nyuma ya miamsho hii. Haiwabadilishi hata kidogo; wakizidi kwenda mbali na Mungu, na kuelekea ulimwenguni, wakati wote. Tazama.

108 Samsoni alijua kilichokuwa kinaenda kutukia ikiwa maombi yake yalijibiwa.

109 Lakini sisi hatujahesabu gharama bado. Ni nini kinachoenda kufanyika kama Mungu akijibu maombi yako kuwa mtoto halisi, wa kweli wa Mungu? Unajua umetoweka kutoka kwenye dhehebu lako, papo hapo. Na hao wanawake ambao mnacheza nao karata, na kila kitu? Loo, la! Umeenda, na ni hayo tu. Afadhali upige hesabu, kwanza.

110 Lakini Samsoni alisema, "Acha nife." Alikuwa tayari kulipa gharama. Pia alijua . . .

111 Sikiza kwa makini sasa tamko hili. Alijua kwamba hali yake ya sasa ya kurudi nyuma isingeweza kukabiliana na changamoto ya wakati huo. Hata hivyo, alikuwa tu mwanamume kadiri alivyowahi kuwa, katika misuli yake. Mwili wake ulikuwa mkubwa tu kama ulivyowahi kuwa. Alikuwa tu ni msuli mkubwa ambao uliweza kuinuka katika mkono wake wakati wowote, labda ulikuwa mkubwa zaidi, kwa sababu alikuwa akifanya kazi ngumu chini katika . . . akifanya kazi nzito zaidi.

112 Tunayo makanisa bora, majengo bora na kila kitu, lakini ziko wapi nguvu zetu, tukinena kiroho? Loo, tungeweza kupiga kura katika taifa. Hakika, tungeweza kufanya mambo haya, lakini hayo—hayo siyo yale ninayozungumzia. Ninazungumza kuhusu Uwepo wa Mungu kutambulishwa miongoni mwetu. Huo ndio tunaopaswa kuishi kwa ajili yake.

113 Alijua kwamba hali yake ya kurudi nyuma isingeweza kukabiliana na changamoto ya wakati huo.

114 Na vivyo hivyo na kanisa linajua sasa. Hatuwezi kulifanya katika hali hii. Huwezi kulifanya. Madhehebu hayathibitishi Neno; hulikana Neno. Dhehebu lenyewe hulikana Neno punde tu linapounda dhehebu. Kitu hicho tu chenyewe, unaenda tu upande ule mwingine, kwa kuanzia. Hulikana Neno. Wakati wote . . .

115 Ninayo maskini dakika moja tu ama mbili, zaidi. Bali tazama, ninapoharakisha sasa na kutimiza neno langu.

116 Wakati wote huku wote walipokuwa wamesimama pale, na mawazo haya yalikuwa yanapitia niani mwao; nami ninatumaini yanatuma baadhi kupitia zenu. Hawakutambua wakati, Samsoni, mawazo yake yalipitia niani mwake. Labda walipitisha chupa, wakapata kinywaji tena. Wanawake wao warembo wa Hollywood walisimama hapo wakiwa na sigara yao kinywani mwao, kama kilikuwa ni kitu kama hicho katika siku hiyo; sidhanii walishuka chini namna hiyo katika siku hiyo. Bali walisimamisha nywele zao na kuchukua kinywaji kingine, na wakipiga makelele, "Halo, Joseph, ama John, ama wewe hapo juu mahali fulani! Tulicheza karata pamoja jana usiku, tulikuwa nje kwenye karamu kubwa." [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

117 "Kuna uwezekano kwamba Mungu atanisikia. Kuna uwezekano." Na wakati alipowaza, Wafilisti hawakuwa wamemtambua, huku mvulana huyu mdogo alikuwa ameifungua mikono yake, akarudi nyuma. Akasema, "Weka mikono yangu juu ya nguzo." "Kuna uwezekano." Loo, jamani!

118 Laiti kanisa lingaliweza kuona hilo. Kuna uwezekano wa uamsho halisi.

119 Alifanya nini? Aliyainua mashimo yake (hakuwa na macho) kumwelekea Mungu. Hawakutambua kucheza kwa midomo yake, wakati alipokuwa akiungama kwa unyofu.

120 Hatuhitaji tu kidogo, "Bwana, nisamehe mimi na Jim, Joe na sisi sote. Amina." Tunahitaji kusafishwa kwa uaminifu, kuanzia mimbarani hadi kwenye bawabu.

121 Kamwe hawakuyaona machozi yakitiririka kutoka kwenye hayo mashimo ambamo wakati mmoja alikuwa na macho. Hawakutambua kucheza kwa midomo yake. Macho yake, machozi yenye chumvi yakitiririka kutoka kwenye mashimo. Alimtaka Mungu afanye Neno Lake kuthibitika mara moja zaidi, kuthibitisha, kama ninavyomwambia huyu Delila leo hii, ama huyu Samsoni, hasa, "Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele!"

122 "Mara moja zaidi," aliwazia, "ingetendeka. Si dhehebu jipya, si mfuasi mpya wa dini potovu, bali Neno lililothibitishwa kutoka Kwako, Mungu! Ninajua Wewe ungali Mungu. Mimi ni kipofu. Nimepotoka. Sistahili kuishi. Jalia nife pamoja na adui huyu. Uliniinua kumwangamiza, nami nimekupungukia, Bwana, bali kuna uwezekano Wewe utanisikia. Mara moja zaidi, Bwana, mara moja zaidi!" Aliomba kwa jitihada kubwa. Alijua kilichokuwa kinakuja. "Bwana, mara hii moja tu zaidi! Mara moja zaidi jalia nimwone Yesu Kristo kama Yeye alivyokuwa jana!" Wakati alipoomba maombi hayo, huku machozi yakitiririka kutoka mashavuni mwake, kwa unyofu mkubwa wa maungamo!

123 Hilo ndilo kanisa linalohitaji. Kiri kwamba umekosea. Sijali yale Daktari Jones asemayo, ama yale mtu yeyote mwingine asemayo. Kama uko nje ya Neno la Mungu, ungama hilo, kwamba uko makosani. Lia kwa sauti, "Mara moja zaidi, Bwana, mara moja zaidi! Mara moja zaidi, Bwana, mara moja zaidi! Lipiza kisasi upofu wangu juu ya madhehebu haya! Na unipe nguvu, Bwana, kuutikisa ulimwengu huu wa madhehebu, kwa thibitisho Lako. Nipe nguvu, Bwana. Mara nyingine zaidi lithibitishe!"

124 Alijua kilichokuwa kinaenda kufanyika kama maombi yake yalijibiwa. Alijua, kwa bidii sana, akilia, "Mara moja zaidi, Bwana!" Ndipo wakati alipokuwa akiomba, na kufanya maungamo yake maaminifu, kila mshipa katika mwili wake ukaanza kuchezacheza.

125 Ee Mungu, kama Mwili wa Yesu Kristo ungeweza kusimama kama mmoja, na kila mshipa na kila kiungo kianze kuchezacheza na ubatizo halisi wa Roho Mtakatifu tena; sio na washiriki wapya, na kupeana mikono, na kanuni fulani ya imani.

126 Wakati nguvu zilipoanza kuingia katika misuli hiyo mikubwa, kila mshipa ulianza kupindika. Alianza kujihisi mwenyewe tena, na akajipinda. Basi, wakati alipojipinda, ukuta huo mkubwa ukaporomoka.

127 Yote tunayohitaji kufanya leo hii, ni, kuona kuta hizi zote za kidhehebu zikiporomoka, ni kuwa wanyofu kabisa mbele za Mungu, kuponya macho haya yaliyopofuka ambayo yamepofushwa yasione Neno la Mungu.

128 Huo ulikuwa ndio ushindi mkubwa kuliko wote wa Samsoni aliowahi kupata, kwa sababu alikuwa tayari kuungama, dhidi ya kila adui kwanza ambaye aliinuliwa kuangamiza.

129 Loo, Pentekoste, simameni mahali penu alasiri ya leo, mahali penu pa wajibu wa Neno la Mungu. Tubuni, na mlie kwa sauti, "Bwana Mungu, mara moja zaidi!" Hebu niwaambieni jambo fulani. Afadhali umwangamize adui wako kabla adui wako hajakuangamiza. Hiyo ni kweli. Rudisheni mikutano ya maombi ya mtindo wa kale, toba halisi ya kitauwa, ibada ya usiku kucha ya madhabahuni. Loo, Pentekoste, nisikieni! Acheni, loo, acheni uozo huu ambao Yezebeli ameingiza miongoni mwenu. Uacheni, uacheni upesi, na mrudi kwenye Neno la Bwana, mbali na maonyesho haya ya Hollywood. Geukeni pamoja na mioyo yenu yote, mrudi kwenye Neno la Mungu. Rudini kwenye Nguvu za Roho Mtakatifu. Enyi wanawake vaeni kama wanawake, enyi wanaume tendeni kama wanaume, kama wana na binti za Mungu. Geukeni, loo, geukeni kutoka kwenye mfumo huu wa Yezebeli unaowasakama na kuwapofusha. Mungu atusaidie kuwa na toba ya kweli; si shingo upande, huwezi kuifanya.

130 Jinsi ninavyowazia leo hii, kwenye wakati huu hasa wakati muda wangu umekwisha, tunapaswa kusimama kwa miguu yetu, na tulie, huku tumeinua mikono yetu hewani, "Bwana, mara moja zaidi! Mara moja zaidi, Ee Bwana, mara moja zaidi!"

131 Hebu tusimame, kila mmoja aliye tayari kusimama, kuona uamsho; ambaye yuko tayari kufia maonyesho haya ya Hollywood; kila mtu aliye tayari kufa, kuona "Nguvu za Mungu zikija Sayuni, na kwa furaha, milima Yake yote mitakatifu hakuna kitu kinachodhuru au kitakachoangamiza."

132 Hebu tuinue mikono yetu, na tulie, "Mara moja zaidi, Bwana!" Mara moja zaidi, Bwana! Mara moja zaidi, Bwana! Mara moja zaidi, Bwana, mtume Roho Mtakatifu, pamoja na Upepo wenye nguvu ukienda kasi kama Wewe ulivyofanya kwenye Siku ya Pentekoste. Amina.

63-0804A Mara Nyingine Tena
Marigold Center
Chicago, Illinois Marekani

SWAHILI

©2020 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:



VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org